

TOLEO LA. 05

# Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025



ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | 4 SEPTEMBER, 2020

## SIMIYU WAMKUBALI MAGUFULI



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



## **DKT. MAGUFULI AWAPA SHULE WAPINZANI KUHUSU MAENDELEO YA VITU**

Na Mwandishi Wetu - **Bariadi - SIMIYU**

Mgombea Urais kwa tiketi ya CCM, Dkt. John Pombe Magufuli ametoa darasa kwa wanasiasa wasiojua umuhimu wa kuwekeza katika vitu ambavyo husaidia kuchochea uchumi na maendeleo ya watu.

“Hakuna nchi yeyote duniani inaweza kuendelea kama haijawekeza katika vitu. Nchi inapotaka kuendelea huanza na vitu ambavyo vitachochea ukuaji wa uchumi,” alifanua Rais Magufuli akiwa Bariadi, Mkoa wa Simiyu alipokuwa akihutubia mkutano wa kampeni kuomba kuchaguliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano kuiongoza Tanzania.

Rais Magufuli alitoa ufafanuzi huo ili kuondoa dhana potofu inayoenezwa na baadhi ya viongozi wa upinzani wanaodai kuwa uwekezaji katika vitu kama vile kununua ndege, ujenzi wa barabara za lami, miradi ya maji, umeme unaofika hadi ngazi ya kijiji, elimu bure, ujenzi wa reli ya kisasa, viwanda na miradi mingine kwamba vyote hivyo havimsaidii mwananchi wa kawaida.



Amefafanua kuwa Serikali yake imewekeza katika miradi mbalimbali ili kuchochea ukuaji wa uchumi unaomfanya mwananchi wa kawaida kunufaika kutokana na uwekezaji huo. Mfano wa miradi ambayo inawanufaisha wananchi ni pamoja na miradi ya maji ambayo imewapunguzia wananchi hususan wakinamama kutumia muda mwingi kutafuta maji na badala yake muda uliokuwa unapotea hivi sasa wanautumia kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Ujenzi wa barabara za lami na ununuzi wa ndege zimesaidia kurahisisha usafiri na usafirishaji kutoka eneo moja hadi lingine na pia kumpunguzia mwananchi gharama za usafiri.

Rais Magufuli amewakumbusha wananchi wa Simiyu adha ya ubovu wa barabara kukosekana kwa huduma muhimu za afya. "Wakati naingia madarakani kulikuwa hakuna barabara wala hospitali na watu walikuwa wanapata shida.

Iliwalazimu watu wa Maganzo kwenda kwanza Mwanza kupitia Lamadi ili wafike hapa Bariadi," Rais Magufuli alikumbusha kuhusu adha hiyo ambapo baada ya uwekezaji katika ujenzi wa barabara kwa sasa wananchi wanasafiri kwa raha na gharama nafuu. Amesema kuwa baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakipinga maendeleo kama ujenzi wa barabara na ununuzi wa ndege na wakati mwingine kutokana, lakini bado wanatumia barabara hizo.

Rais Magufuli ambae amekuwa akivuta umati mkubwa wa watu kila anapoenenda, amewaeleza wananchi wa Bariadi kuwa Serikali inatekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria na ndio maana anaomba wamchague tena pamoja na Wabunge na Madiwani ili kazi ya utekelezaji iendelee kwani endapo watawachagua wapinzani mradi huo unaweza usiendelee kwani wamekuwa wakipinga uwekezaji katika miundombinu ikiwemo miradi ya maji.



# MAFANIKO YA UTENDAJI WA MAGUFULI YATAMBULIKA NA WANA-SIMIYU

Na Mwandishi Wetu - **SIMIYU**



Mkoa wa Simiyu umekuwa na mabadiliko makubwa ikiwa ni takribani miaka mitano tu tangu Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli iingie madarakani mwaka 2015.

Mabadiliko hayo yamegusa sekta mbalimbali ambazo kwa pamoja zimesababisha mabadiliko makubwa kwa kipindi kifupi.

Katika mkutano wake, Mgombea wa Urais wa tiketi cha Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ndiye Jemedari wa kuleta mabadiliko mkoani humo, anaeleza sababu za kufanya maendeleo katika mkoa huo anaeleza kuwa aliona ili ajenge uchumi imara utakaoleta mabadiliko chani aliona ni lazima aanze na vitu vinavyochochea ukuaji wa uchumi.

“Nilipoingia madarakani niliona tutumie mbinu ya kujenga uchumi wa kisasa kwa kuanza na ujenzi wa miundombinu.



Wananchi wa Bariadi walikua wanafariki kwa kukosa huduma za afya karibu na maeneo yao, wagonjwa walikua wakibebwa kwenye tela za ng'ombe, tuliposema lazima Bariadi tujenge hospitali kubwa ya Rufaa watu hawakuamini lakini sasa tumejenga na inatoa huduma," anaeleza Rais Magufuli.

Amewaomba wananchi wa Simiyu kukipa ridhaa Chama cha Mapinduzi kuongoza tena na kuwaahidi katika kipindi cha miaka miwili au mitatu vijiji vyote vya mkoa huo vitakuwa vimeunganishwa na umeme.

"Tumetoka mbali, hata Ulaya hawatoi elimu bure lakini sisi tuliamua kutoa elimu bure kwa

watoto wetu, tumejenga shule 950 za msingi, shule za sekondari 228 na madawati takriban milioni nane nchi nzima.

Tunafanya haya yote kwa kutambua kuwa sisi viongozi tuna jukumu la kutumika, kuongoza ni kuonyesha muelekeo na hki ndicho kitu tunachokifanya kwa maendeleo mapana ya Taifa letu," anaeleza Rais Magufuli.

Rais Magufuli anaongeza: "Hapa Bariadi tume-tumia jumla ya shilingi bilioni 73.8 katika elimu kwa kutengeneza madawati 88,105, madarasa 969, nyumba za walimu na maabara 78 na mabweni 17. Tumekarabati shule kongwe na vyuo viwili, na tumeajiri walimu 1,116 pamoja kununua vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 15.86," anafafanua.

Amesema kuwa shilingi bilioni 206.2 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 117.1 za lami na km 293.4 za changarawe.





Upande wa nishati Rais Magufuli amesema kuwa shilingi bilioni 81.1 zimetumika kutekeleza miradi ya umeme katika vijiji 299 na kwa sasa Serikali inajenga kituo cha kupozea umeme kinachogharimu shilingi bilioni 75.

Amesema kuwa Serikali imeimatisha kilimo, ufugaji na uvuvi, ili wafugaji wasiwe ni watu wa kuhamishwa hamishwa katika Taifa lao.

Pia Rais Magufuli anasema kuwa katika Awamuya Pili ya Uongozi wake atahakikisha vinajengwa viwanda vya pamba ili pamba ichakatwe katika viwanda hivyo kuzalisha bidhaa ambazo zitauzwa nje ya nchi ikiwemo Ulaya.





# MITANO MINGINE YA MAGUFULI KUMWAGA AJIRA 13,000 KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu - Kishapu - SHINYANGA



Sekta ya Elimu itaendelea kupewa kipa-umbele katika miaka mitano mingine ya Serikali ya Awamu ya Tano ambapo Mgombea Urais kwa kupitia Chama cha Mapindizi, Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameahidi kumwaga ajira 13,000 kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.

Rais Magufuli ametoa ahadi hiyo ya kuboresha elimu leo akiwa eneo la Mwigumbi, Wilayani Kishapu mkoani Shinyanga akiwa njiani kuelekea Baria-di mkoa wa Simiyu.

“Ili nchi yoyote duniani iendelee inahitaji uwekezaji kwenye sekta ya elimu, miundombinu kama barabara na reli, afya, maji na mingine ili kufikia maendeleo kama tunavyokwenda nayo sasa,” alisisitiza Rais Magufuli.

Akifafanua amesema kuwa Serikali inaimarisha sekta ya elimu na imetekeleza vizuri mpango wa elimu bure na mpaka sasa imetumia trilioni 1.09 itaendelea kufanya hivyo ili kutoa fursa kwa wataoto wa masikini kupata elimu.



“Tumejenga Kituo cha Afya Mwigumbi ili kuokoa maisha ya akina mama wanaohitaji kufanyiwa upasuaji hapa na hivyo tutakuwa tumefakiwa katika azma yetu yakuendelea kuboresha huduma za jamii na ustawi wa wananchi.

Akizungumzia kuhusu wachimbaji wadogo wa almasi, Rais Magufuli amesema kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa inasimama pamoja na kulinda haki zao.





# BILIONI 7.72 KUJENGA SOKO LA KISASA KIBAHA VIJIJINI

Na Mwandishi Wetu - Mlandizi - PWANI



Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli imetenga zaidi ya shilingi bilioni 7.72 kwa ajili ya ujenzi wa soko jipya la kisasa ambalo litaongeza thamani ya bidhaa zitakazouzwa katika soko hilo.

Mhe. Samia amesema hayo wakati wa mkutano wa kampeni Halmashauri ya Kibaha Vijijini na kuiagiza kutumia fedha hizo ilivyokusudiwa kwani awali fedha hizo zilitengwa na hazikutumika kutokana na kile kinachodaiwa kutoelewana kati ya viongozi na wananchi wa eneo hilo.



"Serikali tuna nia njema na wananchi wote, na ndio maana tumetenga fedha za ujenzi wa soko jipya la kisasa hapa Mlandizi, lakini Halmashauri yenu imeshindwa kulisimamia, matokeo yake wananchi wanalalamika kukosa soko, nawaomba mji-pange, hatupendi kuona wananchi wanapata shida," anaeleza Mhe. Samia.

Aidha, wakazi hao wa Mlandizi walimwambia Mgombea huyo kuwa wanakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa kituo cha mabasi kwenye eneo lao kwani kilichopo sasa, hakina hadhi suala ambalo Mgombea Mwenza huyo alilitolea ufa-fanuzi.

"Wenzenu kwenye maeneo mengine wamepata vituo vya mabasi, lakini hapa Mlandizi mna tatizo, mivutano yenu imesababisha mpaka sasa msijengewe kituo hicho, kaeni muelewane Serikali ya CCM ni sikivu itawajengea kituo hapa," alisisiti-za Mhe. Samia

Amewaahidi wakazi wa Mlandizi kwamba Serikali ya CCM chininya uongozi wa Rais wa sasa, Dkt. John Pombe itaendelea kuboresha maisha ya wananchi hao kwa kujenga miundombinu kwa ajili ya huduma za kijamii.





# 5

## KALI ZA MAGUFULI SIMIYU LEO SEPTEMBER 4, 2020

- 1.** KATIKA NCHI YOYOTE UKITAKA KUJENGA UCHUMI, NI LAZIMA UANZE NA VITU VINAVYOCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI. NILIPOINGIA MADARAKANI NILIONA TUTUMIE MBINU YA KUJENGA UCHUMI WA KISASA KWA KUANZA NA UJENZI WA MIUNDOBINU.
- 2.** TUMETUMIA SHILINGI BILILIANI 206.2 KWA AJILI YA UJENZI WA BARABARA ZENYE UREFU WA KILOMETA 117.1 ZA LAMI NA KILOMETA 293.4 ZA CHANGARAWA KATIKA MKOA WA SIMIYU.
- 3.** TUMETUMIA SHILINGI BILIONI 81.1 KUTEKELEZA MIRADI YA UMEME, TUMEFIKISHA UMEME KATIKA VIJJI 299, BADO TUNAENDELEA NA MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA KUPOZEA UMEME KINACHOGHARIMU SHILINGI BILIONI 75.
- 4.** TUMEIMARISHA KILIMO, UFUGAJI NA UVUVI, ILI WAFUGAJI WASIWE KATIKA TAIFA LA KUHAMISHWA HAMISHWA. TUNATAKA SIKU ZIJAZO TUJENGE VIWANDA VYA PAMBA ILI BADALA YA KUPELEKA PAMBA ULAYA, TUPELEKE BIDHAA ZILIZOTENGENEZWA.
- 5.** UONGOZI UNAPIMWA, SISI MMESHATUPIMA VYA KUTOSHA. SASA TUNAKWENDA KUJENGA KIWANJA CHA NDEGE HAPA SIMIYU.





## **‘MTEMI’ CHENGE AMUAHIDI MAGUFULI USHINDI WA KISHINDO**

Mbunge anayemaliza Muda wake Jimbo la Bariadi, Ndg. Andrew Chenge amemuahidi Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ushindi wa kishindo katika jimbo na mkoa wa Siniyu.

Chenge amesema kuwa watafanya kazi kwa kushirikiana na mbunge aliyeteuliwa kugombea nafasi hiyo ili kuhakikisha ushindi wa kishindo unapatikana katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, 2020. “Naahidi kuwa tumejipanga kufanya kazi kwa pamoja kama timu moja ili kufikia lengo la kumrudisha tena kwa kishindo Rais Magufuli na wabunge wote, madiwani wa Chama cha Mapinduzi CCM”, Alisisitiza Chenge.

Akifafanua amesema Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo inayochangia kuleta ustawi wa wananchi hivyo ni jukumu lake na wenzake kuhakikisha wanafanya kazi ya kuhakikisha kura za kishindo kwa Rais Magufuli.

Mgombea ubunge wa Chama cha Mapinduzi nafasi ya Urais Dkt. John Pombe Magufuli anaendelea na kampeni za kuomba kura kwa wananchi katika mkoa wa Mara ambapo Jumamosi Septemba 5, 2020 kuanzia saa 5:00 asubuhi, Rais Magufuli atafanya kampeni katika Uwanja wa Mkendo, Musoma Mjini.



# VIONGOZI WA DINI SIMIYU WAGUSWA UTENDAJI WA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu - **SIMIYU**



Viongozi wa Dini mkoa wa Simiyu wamemuelezea Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli kwamba mbali na kuwa mchapakazi hodari, kiongozi huyo ni Mchamungu na Mzalendo.

Akimuelezea mgombea huyo wakati wa maombi maalum kabla ya kuanza kwa mkutano wa kampeni kuomba ridha ya wananchi katika nafasi za Urais, Ubunge na Udiwani katika Mkoani wa Simiyu, Askofu wa Kanisa la Mkuu wa Kanisa la Waadiventista wasabato, Mack Malekana amemtaja Rais Magufuli kuwa mtu asi-yeweza kuuzwa wala kununuliwa kwa namna alivyo mzalendo.

“Magufuli ni kiongozi anayechukia mapato ya udhalimu na ni kiongozi mcha Mungu na anayemtanguliza Mungu,” yalisikika sehemu ya maombi ya Askofu Malekana yakieleza wasifu wa Rais wa Magufuli.



Viongozi wa dini walimuomba Kiongozi huyo ili Mwenyezi Mungu amjalie uchaji na hekima zaidi katika kuwatumikia wananchi.

Kwa upande wak,e Shehe Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mahamud Kalokola ame-waomba watazania wote ili waweze kuchagua viongozi wacha Mungu na Wazalendo watakowaitea maendeleo.







## MWENYEKITI UVCCM NAE AWACHAPA WAPINZANI UPOTOSHAJI MAENDELEO YA VITU NA WATU

Na Mwandishi Wetu - **Bariadi - SIMIYU**

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Heri James amesema kuwa Viongozi wa Vyama vya Upinzani wanapotosha wananchi kuhusu dhana ya Maendeleo ya Vitu na Watu.

Akieleza mafanikio yaliyofikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) katika mkoa wa Simiyu, Ndg. James amesema kuwa maendeleo ya watu yanategemea maendeleo ya vitu vinavyofanywa na Serikali kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi.

“Maendeleo ya watu yanategemea vitu kama miundombu ya barabara, reli ya kisasa, Hospitali za kisasa zinazojengwa, miradi ya maji inayotekelezwa, ndege zilizozunuliwa, mifumo ya mawasiliano, viwanja vya ndege, meli zinazojengwa, bandari na vivuko,” ameeleza.

Akifafanua Ndg. James amesema kwa mfano unapojenga reli utasaidia kurahisisha uchukuzi wa abiria na mizigo kutoka eneo moja hadi jingine kwa gharama nafuu hivyo tayari maendeleo ya vitu yatakuwa tayari yamechochea ukuaji wa biashara na ustawi wa watu.





Katika mazingira hayo anabainisha kuwa vitu vinachagiza maendeleo ya watu, hivyo hakuwezi kuwa na maendeleo ya watu bila vitu.

Kwa upande wa meli zinasababisha ufanyaji biashara kuwa rahisi kutoka eneo moja hadi jingine na pia usafishaji wa watu kwa gharama nafuu.

Mwenyekiti huyo wa UVCCM amewataka wananchi kuwapuuza na kutowapigia kura wapinzani ambao wanapinga uwekezaji wa Serikali katika miradi inayochochea ukuajinwa uchumi na kuwaletea wanachi maendeleo.



# Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**